

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: "TUME"
DODOMA
Namba ya Simu: 0738166703
0733005974



Tume ya Utumishi wa Umma,
Jengo la Chimwaga,
Ghorofa ya 2,
2 Barabara ya UDOM,
S.L.P. 1074,
40405 DODOMA.

Barua pepe:
secretary@psc.go.tz
Tovuti: www.psc.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

TAHADHARI YA UTAPELI KUPITIA MITANDAO YA SIMU

Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma kwa nyakati tofauti imepokea taarifa za kuwepo kwa baadhi ya Watu ambao pasipo Tume kujua wamekuwa wakiwapigia simu, kutuma ujumbe "SMS" kwa baadhi ya Maafisa Utumishi na baadhi ya Watu waliowasilisha mashauri na malalamiko yao Tume. Watu hao wamekuwa wakijitambulisha majina na vyeo tofauti kuwa ni Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Umma na wamekuwa wakiomba kupatiwa taarifa mbalimbali za masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma na wengine kuomba kupatiwa fedha.


Taarifa ilizonazo Tume ni kwamba matukio haya yametokea katika Mikoa mbalimbali ikiwemo Kigoma, Morogoro, Dar es Salaam, Tabora na Mtwara.

Ili kutimiza azma yao mbaya ya kuonekana ni Watumishi wa Umma, watu hawa matapeli wamekuwa wakiudanganya Umma na Wananchi kwa kujitambulisha kuwa ni Watumishi wa Serikali kutoka Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, **"Watu hawa ni Matapeli na wapuuzwe"**

Tume inapenda kuufahamisha Umma kuwa tayari hatua stahiki zimechukuliwa na zinaendelea kuchukuliwa dhidi ya Watu hawa. Tume inapenda kuufahamisha Umma kwamba namba mahsusi za simu zinazotumiwa kwa mawasiliano na Tume ni **0738 166 703** na **0733 005 974**, barua pepe ni secretary@psc.go.tz au kufika katika Ofisi za Tume zilizopo Jengo la Chimwaga, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Umma, inaujulisha Umma kuchukua tahadhari dhidi ya Watu hawa na yeyote atakayepigiwa simu yenye viashiria vya utapeli na udanganyifu ni muhimu kutoa taarifa Tume ya Utumishi wa Umma au kuripoti kwenye vyombo vya kiusalama mara moja ili hatua stahiki dhidi ya Watu hawa ziweze kuchukuliwa.

Imetolewa na:



Richard M. Cheyo
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Tume ya Utumishi wa Umma
31 Mei, 2022